JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2022

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2022

# 621 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ........ 2

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu) ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Stadi za Lugha ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Fasihi Simulizi ........ 4
2.1.3 Swali la 3: Sarufi ........ 7
2.1.4 Swali la 4: Utungaji ........ 9
2.1.5 Swali la 5: Sarufi ........ 11
2.1.6 Swali la 6: Mbinu za Kufundishia ........ 15
2.1.7 Swali la 7: Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili ........ 17
2.1.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........ 20
2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili ........ 23
2.1.10 Swali la 10: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili ........ 26
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha ........ 30
2.2.1 Swali la 11: Utungaji ........ 30
2.2.2 Swali la 12: Stadi za Lugha ........ 33
2.2.3 Swali la 13: Upimaji ........ 38
2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili ........ 42

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA ........ 46

4.0 HITIMISHO ........ 47

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 47

KIAMBATISHO CHA PEKEE ........ 49

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limetayarisha taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Cheti Daraja la A katika somo la Kiswahili mwaka 2022. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali.

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Cheti Daraja la A katika somo la Kiswahili mwaka 2022 inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa kizuri. Ufaulu huo, umechangiwa na watahiniwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa na matakwa ya swali, matumizi sahihi ya lugha na alama za uandishi, kutoa hoja sahihi zenye mifano kuntu na kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki. Vilevile, uchambuzi umeonesha kuwa, baadhi ya watahiniwa walipata alama za wastani. Hii imesababishwa na watahiniwa hao kutoa majibu yasiyojitosheleza.

Hata hivyo, watahiniwa wengine walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuandika sehemu za utangulizi na hitimisho hususan katika maswali ya insha.

Baraza linatarajia kuwa, taarifa hii itawawezesha walimu tarajali na wakufunzi kuelewa sababu za watahiniwa kujibu au kutokujibu vizuri maswali mbalimbali. Hivyo, itawasaidia kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na utunzi wa mitihani katika ngazi ya chuo ili kufanya vizuri zaidi katika mitihani itakayotolewa na Baraza la Mitihani.

Baraza la mitihani linatoa shukrani kwa wadau wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.

Athumani S. Amasi

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili ulifanyika mwezi Mei, 2022 ambapo ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Taaluma na Utaalamu wa kufundisha Kiswahili ngazi ya Cheti Daraja la A wa mwaka 2009. Mtihani huu ulikuwa na maswali 14 yaliyogawanyika katika sehemu mbili ambazo ni A na B.

Katika mtihani huu, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kumi na manne (14). Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali kumi (10) katika sehemu A ambapo kila swali lilikuwa na alama 4. Hivyo, kufanya jumla ya alama za sehemu hii kuwa 40. Katika sehemu B, mtahiniwa alipaswa kujibu maswali manne (4) na kila swali lilikuwa na alama 15. Hivyo, kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa 60.

Wakati wa kufanya uchambuzi, ufaulu wa watahiniwa uliwekwa katika viwango vitatu; ambapo kiwango kizuri kilianzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu wa watahiniwa zimeambatanishwa katika kila swali. Viwango vya ufaulu wa watahiniwa vimeainishwa kwa kutumia rangi tatu ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ufaulu hafifu.

Jumla ya watahiniwa 3,663 walisajiliwa kufanya mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2022. Miongoni mwao, watahiniwa 3,617 ambao ni sawa na asilimia 98.8 ya watahiniwa waliosajiliwa walifanya mtihani. Hata hivyo, watahiniwa 46 (1.2%) hawakufanya mtihani. Aidha, watahiniwa wote 3,617 (100%) walifaulu.

Kwa upande mwingine, takwimu hizo zinadhihirisha kwamba, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mtihani huu ni kizuri. Kiwango hicho kimeongezeka kwa asilimia 0.09 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo asilimia 99.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI


### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali kumi (10) yaliyohitaji majibu mafupi ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma na Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na uzito wa alama nne (4). Hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama arobaini (40).

Swali litakuwa limejibiwa vizuri ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa wamepata alama 3 - 4 na litaelezwa kuwa limejibiwa vibaya ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa ndio waliopata alama 0 - 1.5. Aidha, swali litaelezwa kuwa limejibiwa kwa kiwango cha wastani ikiwa idadi ya watahiniwa waliopata alama 2 - 2.5 inazidi theluthi moja (1/3) na haikuzidi theluthi mbili (2/3).


#### 2.1.1 Swali la 1: Stadi za Lugha

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kutaja ujuzi wa aina nne kwa mtiririko ambao ataupata mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao, asilimia 67.5 walipata alama 2 hadi 4 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani. Chati Na. 1 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,644 (45.5%) walijibu swali hili na kupata alama 3 hadi 4 kwani waliweza kukidhi matakwa ya swali kutokana na uelewa mkubwa waliokuwa nao juu ya mada ya *Stadi za Lugha*. Watahiniwa hao waliweza kutaja kwa mtiririko aina 3 hadi 4 za ujuzi ambao anaupata mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili. Ujuzi huo ni: *kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.* Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kulingana na matakwa ya swali.



1 i) Kusikiliza • Ujuzi wa Kusikiliza
ii) Kuzungumza • ujuzi wa Kuzungumza
iii) Kusoma • ujuzi wa Kusoma
iv) Kuandika • ujuzi wa kuandika

**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 1.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 799 (22.1%) walijibu swali hili na kupata alama 2 hadi 2.5. Baadhi yao, walitaja hoja mbili sahihi na hoja nyingine zisizo sahihi na wengine walitaja ujuzi kwa kuchanganya bila kufuata matakwa ya swali ambapo walitakiwa kutaja ujuzi kwa mtiririko kuanzia wa kwanza hadi wa nne. Hata hivyo, katika kutaja huko baadhi yao walipata baadhi ya vipengele na kukosa vipengele vingine hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,174 (32.5%) walipata alama hafifu 0 hadi 1.5 kutokana na uelewa mdogo juu ya ujuzi wanaoupata wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Hivyo, baadhi yao walitaja umuhimu wa kujifunza lugha ya Kiswahili, kama vile: *kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na usahihi, kutumia Lugha ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali, kuthamini lugha ya Kiswahili kama lugha ya Taifa* na *kutamka maneno ya Kiswahili kwa usahihi* badala ya stadi nne za lugha atakazozipata mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili ambazo ni *kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.* Wengine walitaja ujuzi kwa kuchanganya bila kufuata matakwa ya swali ambapo walitakiwa kutaja ujuzi kwa mtiririko kwa kuanzia wa kwanza hadi wa nne na kusababisha kupata

alama hafifu. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja ujuzi wanaoupata wanafunzi wakati wa kujifunza lugha ya Kiswahili.




| | |
|---|---|
| 1 | i) Kuongea Kiswahili kwa ufasaha. |
| | ii) Kutumia alama za uandishi vizuri katika Kusoma au Kuandika |
| | iii) kuelewa vipengele vya taaluma ya Kiswahili vizuri |
| | iv) kutamka maneno kwa usahihi |

**Kielelezo Na.1.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 1.

Kielezo Na. 1.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali kwa kuonesha ufasaha wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuongea, kutumia alama za uandishi, kuelewa taaluma ya Kiswahili pamoja na kutamka maneno kwa usahihi badala ya kutaja ujuzi anaoupata mwanafunzi anayejifunza Lugha ya Kiswahili.


### 2.1.2 Swali la 2: Fasihi Simulizi

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua kwa ufupi wahusika wanne waliomo katika hadithi. Swali lilijibiwa na watahiniwa wote (100%) waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani kwani asilimia 48.1 tu ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 2 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,878 (51.9%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Fasihi Simulizi*. Hii ilisababisha watahiniwa hawa kufafanua wahusika ambao siyo sahihi waliomo katika hadithi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu aina za wahusika kama vile, *wahusika bapa, wahusika mviringo, wahusika wakuu* na *wahusika wadogo wadogo*. Wengine walitoa majibu kama vile, *muhusika mkuu*, *muhusika msaidizi, muhusika anayebadilika badilika* na *muhusika asiyebadilika badilika* badala ya kutaja wahusika kama vile*: msimulizi ambaye ndiye msimuliaji wa hadithi, wasikilizaji ambao ndio wapokeaji wa hadithi inayosimuliwa, wanyama ambao hutumika kama wahusika wanaowakilisha sifa za binadamu, vitu na mahali ambao hawa ndio mizimu, mazimwi, mibuyu,vichaka, mapango na makaburi* Wengine waliandika *wahusika wakuu, wahusika chipukizi, wahusika wakongwe* na *wahusika wadogowadogo.* Pia baadhi ya watahiniwa walitaja baadhi ya wahusika sahihi na kupata alama za kiwango hafifu. Kielelezo Na 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua kwa usahihi wahusika wanne wanaopatikana katika hadithi kwa kujibu kinyume na matakwa ya swali.



2
Haditi ya watoto wa mama ntilie
Wahusika
- Mama ntilie
Mchapakazi, Mtunza familia, mnyonge
- Mzee lomolomo
Mume wa mama ntilie, mlevi, hajishug-
hulishi
- Zita
Binti wa mama ntilie, maskini, mpambanaji
- Peter
Kijana wa mama ntilie, mpambanaji,
mwenye huruma

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 2.

Kielelezo Na. 2.2, kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye alijibu kinyume na matakwa ya swali kwani alifafanua kwa ufupi wahusika wanaopatikana katika Riwaya ya *Watoto wa Mamantilie* badala ya kufafanua wahusika waliomo katika hadithi. Wahusika hao ni kama vile, Mama Ntilie, Mzee Lomolomo, Zita na Peter.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 264 (7.3%) walipata alama 2 hadi 2.5. Miongoni mwao, walishindwa kuchambua kwa usahihi baadhi ya wahusika wanaopatikana katika hadithi hivyo, kupata alama za wastani. Vilevile, watahiniwa wengine walitaja baadhi ya wahusika bila kuchambua hoja zao kama yalivyokuwa matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine watahiniwa 1,475 (40.8%) waliofanya swali hili na kupata alama 3 hadi 4, waliweza kuchambua kwa ufupi wahusika 3 hadi 4 wanaopatikana katika hadithi. Hii inathibitisha kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fasihi Simlizi*. Majibu yaliyotolewa na watahiniwa hawa ni kama vile: *msimulizi ambaye ndiye msimuliaji wa hadithi, wasikilizaji ambao ndio wapokeaji wa hadithi inayosimuliwa, wanyama ambao hutumika kama wahusika wanaowakilisha sifa za binadamu, vitu na mahali ambao hawa ndio mizimu, mazimwi, mibuyu,vichaka, mapango na makaburi*. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuchambua kwa usahihi wahusika wanaopatikana katika hadithi.




| 2 | i) Fanani, Ni msimuliaji wa hadithi |
|---|---|
| | ii) hadhira, Ni msikilizaji wa hadithi |
| | iii) Wanyama kuna baadhi ya hadithi zinatumia wanyama kama fisi, simba, mbwa katika kuwasilisha |
| | iv) Binadamu pia kuwepo hadithi kunaweza kutawa na majina ya watu |

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2.

### 2.1.3 Swali la 3: Sarufi


Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kuchagua neno sahihi kutoka katika orodha ya maneno yaliyopo katika kisanduku na kukamilisha muundo wa sentensi nane alizopewa. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Miongoni mwao, asilimia 99.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili ndio waliopata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango kizuri kama inavyoonekana katika chati Na. 3**.**




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 3,440 (95.1%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu huo ulitokana na uelewa mkubwa waliokuwa nao juu ya mada ya *Sarufi*. Hivyo, waliweza kuchagua neno sahihi kutoka katika orodha ya maneno yaliyopo katika kisanduku na


kukamilisha miundo ya sentensi walizopewa. Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa wa kundi hili wana umahiri na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Sarufi* pengine kutokana na mada hiyo kufundishwa kuanzia elimu ya msingi. Kielelezo Na 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyeweza kuchagua neno sahihi kutoka katika orodha ya maneno aliyopewa na kukamilisha miundo ya sentensi alizopewa.




**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 3.

Vilevile, watahiniwa 173 (4.8%) walipata alama 2 hadi 2.5. Miongoni mwao, walichagua maneno sahihi kuanzia 4 hadi 5 kutoka katika orodha ya maneno yaliyopo katika kisanduku na kukamilisha miundo ya sentensi 4 hadi 5 kwa usahihi. Pia, watahiniwa wengine walikamilisha baadhi ya sentensi kwa usahihi na kushindwa katika sentensi nyingine kwa kutumia maneno ambayo hayapo kwenye kisanduku kinyume na matakwa ya swali hivyo, kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana (0.1%) walipata alama hafifu. Watahiniwa hao, walishindwa kuchagua maneno sahihi kutoka katika kisanduku na kukamilisha sentensi ili ilete maana. Miongoni mwao, walichagua baadhi ya majibu sahihi na kupata alama za kiwango hafifu. Kwa ujumla watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Sarufi* hivyo, kushindwa kukamilisha sentensi kwa kuchagua neno sahihi kulingana na muundo wa sentensi husika. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali husika.




| | |
|---|---|
| 3 | (a) . ingawa |
| | (b) - Hawa |
| | (c) - isipokuwa |
| | (d) - Aa Baada ya |
| | (e) - na |
| | (f) . Kwa |
| | (g) - Ndio |
| | (h). Baadaye |
| | |

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 3.

Kielelezo Na. 3.2, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyekosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Sarufi* kwani alichagua maneno ambayo siyo sahihi katika kukamilisha miundo ya sentensi alizopewa. Hata hivyo alichagua majibu sahihi katika kipengele (b), (d) na kipengele (f) hivyo, kupata alama za kiwango hafifu.

### 2.1.4 Swali la 4: Utungaji


Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kutaja mambo manne ya kuzingatia ili kusaidia utungaji wa maandishi kuwa bora zaidi. Wanafunzi wote (100%) walijibu swali. Kati yao, asilimia 29.6 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 na kusababisha swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 2,547 (70.4%) walipata alama 0 hadi 1.5 kwani hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mambo ya

kuzingatia ili kusaidia utungaji wa maandishi kuwa bora zaidi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hatua za kufuata wakati wa kuandika utungaji wa maandishi kama vile: *kukusanya mawazo, kuchagua mawazo, kupanga mawazo na kuendeleza mawazo* badala ya kutaja mambo ya kuzingatia ili kusaidia utungaji bora wa maandishi ambayo ni: *Kuelewa vyema maana ya msingi ya mada husika, mtumiaji kuwa na msamiati wa kutosha, kuzingatia mtiririko wa mawazo unaoleta mantiki* pamoja na *kuzingatia alama mbalimbali za uandishi*. Wengine waliandika vitu vya msingi vinavyosaidia utungaji wamaandishi kuwa bora kama vile; *kichwa cha somo kinachofaa, utangulizi, kiini na hitimisho.* Vilevile, wengine walitoa hoja kama *kuwepo kwa wataalamu wa kutosha, kuwepo kwa vitendea kazi muhimu, kuwepo kwa miundombinu mizuri* na *kutambua umuhimu wa maandishi bora*. Kwa ujumla, watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Utungaji* hivyo, kutoa hoja kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na 4.1 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali husika.


4 i) Vifaa vya utungaji
ii) Mwandiko mzuri
iii) Uzingatiaji wa vituo.
iv) Mkorezo wa rangi za maandishi


**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 4.

Katika kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alishindwa kutaja mambo sahihi manne ya kuzingatia ili kusaidia utungaji wa maandishi kuwa bora zaidi. Mtahiniwa huyo alitoa hoja ambazo ni kinyume na matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 937 (25.9%) walifanya swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Miongoni mwao, walimudu kutaja jambo 1 hadi 2 sahihi ya kuzingatia ili kusaidia utungaji wa maandishi kuwa bora zaidi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama (i) *misamiati,* (ii) *miundo,* (iii) *matumizi ya herufi kubwa* na (iv) *alama za uandishi.* Mtahiniwa huyo aliweza kupata hoja katika kipengele cha (i) na cha (iv). Halikadhalika, watahiniwa wengine wa kundi hili walitoa hoja kama vile: (i) *maana ya maneno,* (ii) *kuzingatia alama bora za uandishi,*

(iii) *kuzingatia sarufi ya neno* na (iv) *mpangilio mzuri wa mawazo*. Katika majibu hayo mtahiniwa aliweza kutoa majibu sahihi katika kipengele cha (ii) na (iv), hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa 133 (3.7%) walipata alama 3 hadi 4 kwani walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mambo manne ya kuzingatia ili kusaidia utungaji wa maandishi kuwa bora zaidi. Watahiniwa hao, waliweza kutaja mambo hayo kama vile: *Kuelewa vyema maana ya msingi ya mada husika, mtumiaji kuwa na msamiati wa kutosha, kuzingatia mtiririko wa mawazo unaoleta mantiki* pamoja na *kuzingatia alama mbalimbali za uandishi*. Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na umahiri na maarifa ya kutosha katika mada ya *Utungaji*. Kielelezo Na 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi swali husika.


4

(i) Lugha fasaha

(ii) Uzingatie alama za uandishi.


(iii) Uelewa wa Mada.

(iv) Mpangilio mzuri wa matukio au visa.

**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4.


### 2.1.5 Swali la 5: Sarufi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa tofauti za aina za maneno kati ya (a) kiwakilishi na kivumishi na (b) kiunganishi na kihusishi. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili ambapo asilimia 76.5 walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Watahiniwa 1,491 (41.2%) walijibu swali hili vizuri na kupata alama 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Sarufi* hususani katika aina za maneno. Hivyo, waliweza kutofautisha aina za maneno kati ya kiwakilishi na kivumishi pamoja na kiunganishi na kihusishi huku baadhi wakitoa mifano. Mtahiniwa mmoja aliandika kuwa, Kiwakilishi *ni neno linalofanya kazi ya nomino kama nomino haikutajwa bayana* kwa mfano, ***Wale*** *wanaimba wimbo* lakini kivumishi ni *neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi* kwa mfano, *mtoto* ***mzuri*** *amelazwa leo.* Pia, kiunganishi ni *maneno yanayotumika kuunganisha dhana mbili au zaidi katika sentensi* kwa mfano, *mbuzi ameanguka* ***ingawa*** *hajaumia* lakini kihusishi ni *maneno yanayotumika kuonesha uhusiano uliopo baina ya neno moja na mengine* kwa mfano, *nitafika* ***kwa*** *Juma*. Aidha, watahiniwa hawa waliweza kutoa mifano ya maneno katika kila aina ya neno. Kielelezo Na 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutofautisha dhana hizo kwa usahihi.


5

a) Kiwakilishi; ni maneno yanayosimama badala ya nomino; mfano; Yule, wale, mimi na sisi.

Lakini.

Kivumishi; ni aina ya maneno yanayoelezea sifa aliyonayo mtu au kitu fulani; mfano; mnene, Mzuri na mrefu.

b) Kiunganishi; ni aina ya maneno yanayounganisha neno na neno au sentensi na sentensi. mfano; Juma analima na mama anapika.

Lakini.


Kihusishi; ni aina ya maneno yanayoonesha uhusiano wa kitu fulani. mfano.
Emmanuel anatembea kwa miguu.

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 5.

Aidha, watahiniwa 1,276 (35.3%) walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kutokana na uelewa wa wastani waliokuwa nao juu ya aina za maneno. Hivyo, waliweza kutoa hoja za kutofautisha zisizojitosheleza na wengine walitoa mifano bila kufafanua dhana husika na kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa tofauti ya kiwakilishi na kivumishi kuwa, kiwakilishi *ni maneno yanayowakilisha nomino mfano, loo! na kwa* wakati kivumishi *ni maneno yanayovumisha nomino mfano alikuwa na huwa*. Katika majibu hayo, mtahiniwa aliweza kutoa maana sahihi ya kiwakilishi na kivumishi na kushindwa kutoa mifano sahihi. Katika kutofautisha kiunganishi na kihusishi mtahiniwa alieleza kuwa, kiunganishi *ni maneno yanayounganisha neno kwa neno au sentensi na sentensi mfano na* na *lakini*. Wakati kihusishi *ni maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi na kutoa mifano kama vile, vizuri* na *haraka*. Katika majibu hayo mtahiniwa alitoa maana sahihi ya kiunganishi na mifano na kushindwa kutoa maana sahihi ya kihusishi ambapo maana ya kihusishi iliyotolewa inaelezea aina ya maneno inayoitwa "kielezi." Kwa ujumla watahiniwa wa kundi hili wanaelewa baadhi ya aina ya maneno tu.

Hata hivyo, watahiniwa 850 (23.5%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za maneno mbalimbali hivyo, walishindwa kutofautisha aina za maneno walizopewa.

Kwa mfano, katika kutofautisha kiwakilishi na kivumishi, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa: kiwakilishi *huelezea tendo lilivyofanyika* badala ya neno linalofanya kazi ya nomino kama nomino haikutajwa bayana wakati kivumishi *huelezea mtendwa wa jambo* badala ya *neno linalotoa taarifa ya zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi* kwa mfano, *mtoto* ***mzuri*** *amelazwa leo.* Aidha, mtahiniwa huyo aliendelea kutofautisha kiunganishi na kihusishi kuwa, kiunganishi *huelezea sifa ya ziada ya nomino* badala ya *maneno yanayotumika kuunganisha dhana mbili au zaidi katika sentensi* kwa mfano, *mbuzi ameanguka* ***ingawa*** *hajaumia* wakati alieleza kihusishi kuwa *ni sentensi zinazoelezea mtu au mahali* badala ya *maneno yanayotumika kuonesha uhusiano uliopo baina ya neno moja na mengine* kwa mfano, *nitafika* ***kwa*** *Juma*. Kwa ujumla tofauti zilizotolewa na mtahiniwa huyu haziko bayana. Hivyo zilionesha ni jinsi gani watahiniwa walivyokosa umahiri na maarifa juu ya mada ya Sarufi hususani katika aina za maneno. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


5
(a) -Kiwakilishi huwakilisha Kitu flani eg.

- Kivumishi - Hutaja sifa za Kitu flani

(b) -Kiunganishi ni muungano wa sentensi mbili.


- Kihusishi Ni sentensi zinazo elezea umiliki wa Kitu au mtu

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5.

Kielelezo Na. 5.2 ni majibu ya mtahiniwa ambaye badala ya kutofautisha aina za maneno alizopewa alitoa maana zisizo sahihi za aina hizo kinyume na matakwa ya swali. Pia, alikuwa na makosa ya kitahajia kwa mfano flani badala ya fulani.

### 2.1.6 Swali la 6: Mbinu za Kufundishia na Kujifunza Kiswahili

Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze kwa ufupi manufaa manne anayoyapata mwalimu anapofundisha kwa kutumia onesho mbinu wakati wa kufundisha somo la Kiswahili. Asilimia 97.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 264 (7.3%) walijibu swali hili vizuri na kupata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hawa waliweza kueleza kwa ufupi manufaa manne anayoyapata mwalimu anapofundisha kwa kutumia onesho mbinu wakati wa kufundisha somo la Kiswahili. Hii inadhihirisha walikuwa na maarifa na umahiri wa kutosha wa kubaini umuhimu wa kutumia onesho mbinu katika kufundishia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza manufaa kama vile; *kumsaidia mwalimu kueleweka kwa urahisi*, *mwalimu hufanya mwanafunzi kutenda kwa ufanisi*, *humsaidia mwalimu kuvuta usikivu kwa wanafunzi* na *humsaidia mwalimu kufikia malengo aliyoyapanga*. Kielelezo Na 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza manufaa manne anayoyapata mwalimu anapofundisha kwa kutumia onesho mbinu.



6 Manufaa ya kutumia onesho mbinu kwa mwalimu ni kama:-

i) kumsaidia mwalimu kueleweka kwa urahisi. hasa kwa wanafunzi wenye matatizo ya kusikia.

ii) Mwalimu hufanya mwanafunzi kutenda jambo kwa Ufanisi hii ni kutokana na kuona mwalimu anachofanya.

iii) Humsaidia mwalimu kuvuta usikivu kwa wanafunzi.

iv) Humsaidia mwalimu kufikia malengo aliyopanga kuyafikia katika kipindi hicho.


**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6.

Kielelezo Na. 6.1, kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye alijibu vizuri swali kwa kueleza manufaa anayoyapata mwalimu anapofundisha kwa kutumia onesho mbinu wakati wa kufundisha somo la Kiswahili.

Vilevile, watahiniwa 3,270 (90.4%) walifanya swali hili na kupata alama 2 hadi 2.5 kutokana na uelewa wa wastani waliokuwa nao kuhusiana na manufaa anayoyapata mwalimu anapofundisha somo la Kiswahili kwa kutumia onesho mbinu. Miongoni mwao, walitoa hoja zisizojitosheleza na wengine walitoa hoja 2 badala ya 4 kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Hivyo, kutokana na majibu hayo, watahiniwa wengi walipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 83 (2.3%) walipata alama 0 hadi 1.5 kwa sababu walikuwa na uelewa mdogo juu ya manufaa anayoyapata mwalimu anapofundisha somo la Kiswahili kwa kutumia onesho mbinu. Hivyo, walitoa hoja dhaifu kama vile: *husababisha mwalimu kuwa mkali, mwalimu kupendelea baadhi ya wanafunzi darasani kwenye kuuliza maswali, mwalimu kutumia muda mrefu* na *mwalimu kutumia gharama nyingi ya kifedha* badala ya *kumsaidia mwalimu kueleweka kwa urahisi, mwalimu hufanya mwanafunzi kutenda kwa ufanisi, humsaidia mwalimu kuvuta usikivu kwa wanafunzi* na *humsaidia mwalimu kufikia malengo*

*aliyoyapanga*. Watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali kwani walielezea manufaa anayoyapata mwanafunzi badala ya manufaa anayoyapata mwalimu akitumia onesho mbinu katika kufundisha somo la Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa onesho mbinu *humsaidia mwanafunzi kuwa na hamu ya kuingia darasani, kustarehesha, kukuza utamaduni* na *kuwa mzaleno.* Kwa ujumla, mtahiniwa huyu alishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo, kutoa majibu yasiyo sahihi. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali husika.


6

i) Kujengea mwanafunzi kumbukumbu za kudumu

ii) Kuibua vipaji vya wanafunzi

iii) Kuburudisha


iv) Kuelimisha

**Kielelezo Na. 6.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6.

Kielelezo Na. 6.2, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja ambazo haziendani na matakwa ya swali kwa kuonesha baadhi ya dhima za Fasihi Simulizi badala ya kueleza kwa ufupi manufaa anayoyapata mwalimu anapofundisha somo la Kiswahili kwa kutumia onesho mbinu.


### 2.1.7 Swali la 7: Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuelezea kwa ufupi sifa za picha na michoro inayopaswa kuwepo katika kitabu cha kiada cha mwanafunzi wa shule za msingi. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani, walijibu swali hili. Miongoni mwao asilimia 82.5 walipata alama 2 hadi 4 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Watahiniwa 1,817 (50.2%) walijibu swali hili vizuri na kupata alama 3 hadi 4 kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sifa za picha na michoro inayopaswa kuwemo katika kitabu cha kiada cha mwanafunzi wa shule ya msingi. Watahiniwa hao, waliweza kutaja sifa sahihi 3 hadi 4 kulingana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile: *kipakwe rangi nzuri na kwa mpangilio, mchoro uwe wenye uhalisia wa jambo, mchoro uwe mkubwa na wenye kuonekana vizuri* na *mchoro uwe wenye kumfikirisha mwanafunzi.* Kwa ujumla, watahiniwa wa kundi hili walikuwa na umahiri na mawanda mapana kuhusu sifa za picha na michoro inayopaswa kuwepo katika kitabu cha kiada. Kielelezo Na 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja sifa nne za picha na michoro inayopaswa kuwepo katika kitabu cha kiada cha mwanafunzi wa shule ya msingi.


7

(a) Kipakwe rangi nzuri na kwa mpangilio pici pi mchoro usiwe na rangi inayoumiza macho.

(b) Mchoro uwe wenye uhalisia wa jambo, kitu bu cha kiada kionyeshe shughuli / vitu mfano kufyeka majani, meza, viti

(c) Mchoro uwe mkubwa, wenye kuonekana vizuri kwa wanafunzi na uweze kueleweka.


(d) Mchoro uwe wenye kumfikirisha mwanafunzi mfano mwalimu kutoa zoezi la kwenye kitabu kuhusu kutazama picha na kujibu maswali.

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,167 (32.3%) walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani kuhusu sifa za picha na michoro inayopaswa kuwepo katika kitabu cha kiada cha mwanafunzi wa shule ya msingi. Baadhi ya watahiniwa walitaja sifa 1 hadi 2 kwa usahihi hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *iwe na muonekano mzuri, iendane na lengo kuu au maudhui ya somo husika, inatakiwa iwe mikubwa na inatakiwa isiwe na lugha ya mficho*. Katika majibu hayo, mtahiniwa alitoa hoja sahihi katika hoja ya kwanza na ya pili japokuwa alishindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza.

Hata hivyo, watahiniwa 633 (17.5%) walijibu swali hili na kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa wa kundi hili walikuwa na uelewa mdogo kuhusu sifa za picha na michoro inayopaswa kuwepo katika kitabu cha kiada cha mwanafunzi wa shule ya msingi. Hivyo, walishindwa kuelezea sifa hizo kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika sifa za jumla za kitabu cha kiada badala ya sifa za picha na michoro inayopaswa kuwepo katika kitabu cha kiada ambazo ni: *utoshelevu wa maudhui*, *kiwe na lugha rahisi na kueleweka kwa wanafunzi*, *kiwe na mazoezi yatakayomsaidia mwanafunzi katika kujifunza kwake* na *kinaweza kuwa ni gazeti*. Aidha, watahiniwa wengine walitaja hoja kama vile, *kiwe na mada zinazopatikana katika muhtasari wa somo la Kiswahili, kiwe na lugha ambayo siyo fasaha ya Kiswahili, kiwe na mazoezi na mifano ya kutosha* na

*kiwe kimepangwa katika mtiririko mzuri*. Watahiniwa wengine walitaja hoja moja sahihi na nyingine zisizo sahihi na kusababisha kupata alama 1. Kielelezo Na 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja sifa nne za picha na michoro inayopaswa kuwepo katika kitabu cha mwanafunzi.


7

i) Kitabu cha kiada kinatakiwa Mada zote kama inayooneshwa Katika Muhtasari

ii) Kitabu cha kiada kiwe chepesi na lugha sahihi inayoeleweka

iii) Kitabu cha kiada kiwe na Mazoezi Mengi na ya kutosha


iv) Kitabu cha kiada kiwe jalada gumu

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7.

Kielelezo Na. 7.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeandika sifa za kitabu cha kiada badala ya sifa za picha na michoro inayotakiwa kuwepo kwenye kitabu hicho.


### 2.1.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kutaja namna nne zinazoweza kutumiwa na mwalimu ili kupata zana bora za kufundishia na kujifunzia. Watahiniwa wote (100%) waliofanya mtihani walijibu swali hili ambapo asilimia 95.4 walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 8 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 3,129 (86.5%) walijibu swali hili na kupata alama 3 hadi 4 kwani waliweza kutaja namna nne zinazoweza kutumiwa na mwalimu ili kupata zana bora za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliainisha namna hizo kuwa: *kufaragua*, *kuokota*, *kununua* na *kuazima*. Kwa ujumla, majibu yao yanadhihirisha kuwa watahiniwa hawa walipata maarifa ya kutosha kuhusu Mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia hivyo kuweza kujibu swali kwa usahihi. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa mmoja wapo.



8

Mwalimu ataweza kupata zana bora za kufundishia na kujifunzia kwa namba mbalimbali ambazo.

i) Kufaragua - atafaragua zana kutumia makunzi mbalimbali yanayopatikana katika mazingira.

ii) kuokota - atookota maku zana au kuokota makunzi yakutengenezea zana yako.

iii) Kununua - anaweza kununua zana dukani au kwa mtu mwenye zana hiyo.

iv) Kuazima - anaweza kuazima kwa mtu mwenye nayo na baada ya kumaliza kuitumia atarudisha kwa muhusika.


**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 322 (8.9%) walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani kuhusu Mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia hivyo kupata alama 1 hadi 2. Kwa mfano mtahiniwa mmoja, aliandika baadhi ya hoja sahihi kama vile, *kutengeneza*, *kuchonga*, *kuchora na kununua.* Aidha, katika majibu hayo mtahiniwa alitoa majibu sahihi katika hoja ya kwanza na ya nne na kukosa hoja ya pili na ya tatu. Hivyo, kusababisha kupata alama za wastani. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile, *kufaragua*, *kununua*, *kuchonga* na *kufinyanga*. Hata hivyo katika majibu hayo mtahiniwa alitoa majibu sahihi katika hoja ya kwanza na ya pili na alikosa katika hoja ya tatu na nne.

Hata hivyo, watahiniwa 166 (4.6%) walipata alama 0 hadi 1.5. Wengi wao, walikosa uelewa juu ya Mada ya Kufundishia na Kujifunzia. Hivyo, kushindwa kutaja namna nne zinazoweza kutumika na mwalimu ili kupata zana bora za kufundishia na kujifunzia. Mtahiniwa mmojawapo alieleza kuwa namna bora ya kupata zana za kufundishia na kujifunzia ni kupitia vifaa vya mtaala kama vile: *kutokana na andalio la somo katika kufundishia,*

*kutokana na azimio la kazi katika kufundishia, kutokana na nukuu za somo katika kufundishia* na *kutokana na muhtasari wa somo katika kufundishia* badala *ya kufaragua, kuokota, kununua* na *kuazima.* Mtahiniwa huyu alishindwa kuelewa kuwa swali lilitaka njia anazoweza kutumia mwalimu kupata zana bora na si vifaa vya mtaala vinavyoonesha zana za kufundishia na kujifunzia mada mbalimbali.

Aidha, watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika umuhimu wa kutumia zana badala ya kuandika namna bora ya kupata zana za kufundishia na kujifunzia. Hivyo, kutokana na majibu hayo, inadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikosa umahiri juu ya zana ya kufundishia na kujifunzia. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa zana bora za kufundishia na kujifunzia.


8

a) Kupitia sayansi na teknolojia.

b) Mazingira yalotuzunguka.

c) Vyombo vya mawasiliano mfano; Redio, Majarida.


d) Usomaji wa vitabu mbalimbali.

**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 8.

Kielelezo Na. 8.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja namna nne zinazoweza kutumika na mwalimu ili kupata zana bora za kufundishia na kujifunzia badala yake aliainisha namna tatu zinazoweza kumsaidia mwalimu kupata maudhui ya mada fulani katika hoja (a), (c) na (d). Hata hivyo, alitaja eneo ambalo zana huweza kupatikana katika hoja (b) mazingira halisi badala ya namna.


### 2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa ufupi hatua nne ambazo mwalimu anapaswa kuzifuata kufundishia somo la kusoma kimya kwa wanafunzi wa Darasa la Tano. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yenye ufaulu hafifu kwani asilimia 16.6 tu ndio walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 83.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya hatua nne ambazo mwalimu anapaswa kuzifuata anapofundisha somo la kusoma kimya. Watahiniwa wengi walitoa ufafanuzi bila kuzingatia somo husika hivyo, kutoa majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza mambo ya kuzingatia wakati wa kusoma kimya Kama vile: *kutambulisha somo, kuwafundisha misamiati migumu iliyopo katika usomaji huo, wasome pasipo kuchezesha midomo* pamoja na *wasome bila kupepesa vidole juu ya maandishi* badala ya kufafanua hatua zinazopaswa kufuatwa na mwalimu anapofundisha somo la kusoma kimya ambazo ni: *kuchagua kifungu cha habari, kueleza maudhui na umuhimu wa habari hiyo, kuwaelekeza wanafunzi namna ya kusoma kimya kuwapa wanafunzi muda wa kutosha wa kusoma na kurudia ili kupata dhana iliyokusudiwa.* Watahiniwa wengine waliandika maarifa watakayopata wanafunzi baada ya kusoma somo la kusoma kimya kama vile: *wanafunzi wajue maana ya kusoma kimya, wajue umuhimu wa kusoma kimya, kutambua faida ya usomaji kimya na kutambua aina za usomaji.* Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.


9 Hatua anazotakiwa kufuata mwalimu anapo fundisha somo lake:-

@ Utangulizi
Mfano kuimba nyimbo, kuuliza maswali ya mdomo, chemshabongo.

b) Kujenga umahiri (Maarifa mapya)

c) Kuimarisha umahiri (kukazia maarifa)

d) Hitimisho
Mfano kutoa zoezi, kuuliza maswali juu ya kile alichofundisha.


**Kielelezo Na.9.1:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 9.

Kielelezo Na. 9.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali ambapo mtahiniwa alitaja baadhi ya vipengele vya andalio la somo badala ya hatua ambazo mwalimu anapaswa kuzifuata anapofundisha somo la kusoma kimya kwa wanafunzi wa Darasa la Tano.

Licha ya watahiniwa wengi kupata alama za kiwango hafifu, watahiniwa 510 (14.1%) walijibu swali hili na kupata alama 2 hadi 2.5 kwa kuwa walikuwa na uelewa wa wastani juu ya hatua za kufuata mwalimu anapofundisha somo la kusoma kimya. Hivyo walieleza kwa ufupi hoja 1 hadi 2 ambazo mwalimu anapaswa kuzifuata anapofundisha somo la kusoma kimya. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika: *kuliweka darasa katika hali ya utulivu, kuchagua kifungu cha habari, kumtaka mwanafunzi asome kimya pasipo kutamka neno au sentensi kwa sauti* na *kuwataka wanafunzi watoe ufupisho wa kile walichosoma katika kifungu hicho cha habari.* Aidha, katika majibu hayo mtahiniwa alitoa majibu sahihi katika hoja ya pili na ya tatu na kukosa hoja ya kwanza na ya nne hivyo, kusababisha kupata alama za wastani. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile: *kuandaa kifungu cha habari*, *mwalimu kusoma kifungu hicho na kubaini misamiati iliyomo*, *kuwaruhusu wanafunzi kusoma habari hiyo bila kutoa sauti* na *mwalimu na wanafunzi kuchambua misamiati iliyomo katika*

*habari hiyo*. Hata hivyo, katika majibu hayo mtahiniwa alitoa majibu sahihi katika hoja ya kwanza na ya tatu na kukosa katika hoja ya pili na ya nne.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 92 sawa na asilimia 2.5% walipata alama 3 hadi 4 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kufundisha somo la kusoma kimya. Watahiniwa hao, waliweza kuelezea kuwa ili somo hilo liweze kufundishwa vizuri hatua zifuatazo hazina budi kufuatwa; *kuchagua kifungu cha habari, kueleza maudhui na umuhimu wa habari hiyo, kuwaelekeza wanafunzi namna ya kusoma kimya* na *kuwapa wanafunzi muda wa kutosha wa kusoma na kurudia ili kupata dhana iliyokusudiwa*. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali.


9

i) kuandaa kifungu cha habari, mwalimu aandike / atafute habari ~~atayo~~ atakayo itumia kufun-dishia.

ii) kuwaelekeza wanafunzi madhumuni ya kusoma, Mwalimu anatakiwa awaambie wanafunzi kitu wanachoenda kukisoma kinahusu nini

iii) kuwaelekeza wanafunzi namna ya kusoma, mwalimu anatakiwa kuwaambia wanafunzi wake namna ya kusoma hiyo habari je wasome kwa sauti au kimya kimya

iv) kutoa muda wa kusoma, Baada ya mwalimu kuwaelekeza namna ya kuso-ma sasa anatakiwa kuwapa muda wa kusoma habari.


**Kielelezo Na.9.2:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 9.

Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeelewa swali vizuri na kujibu vizuri ambapo alitoa hoja zote sahihi.

### 2.1.10 Swali la 10: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili


Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuchambua changamoto nne ambazo zinaweza kutokea endapo mwalimu atatumia mbinu ya kualika mgeni katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa (100%) walijibu swali hili, ambapo asilimia (98.2%) walipata alama 2 hadi 4. Swali hili ni

miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri, Chati Na. 10 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa watahiniwa 2,938 (81.2%) walijibu swali hili na kupata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Mada ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia kiswahili hususani katika mbinu ya kualika mgeni. Hivyo, waliweza kuchambua changamoto nne zinazoweza kujitokeza iwapo mwalimu atatumia mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *mwanafunzi anaweza kutokujiamini kutokana na kuona mgeni anawafundisha, somo linaweza kutoeleweka kutokana na utofauti wa uwasilishwaji, somo halitafikia malengo mahususi kutokana na mgeni anakuwa hawajui wanafunzi na hajawazoea* na *watoto wenye mahitaji maalumu hawatamuelewa mgeni kutokana na mgeni kutowajua na kuwazingatia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile: *wanafunzi kumshangaa mgeni badala ya kusikiliza kinachofundishwa, kushindwa kulimudu darasa, wanafunzi kutoelewa somo kutokana na njia ambazo wamekwishazizoea* na *wanafunzi kuogopa kuuliza maswali*. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuchambua kwa usahihi changamoto nne za kutumia mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji somo la Kiswahili.


10


i. Wanafunzi kumshangaa mgeni badala ya ku
sikiliza kinachofundishwa. Kutokana na hawaja
wahi ~~kuo~~ kumuona kabda ni mara yao ya
kwanza hivyo ni lazima washangae.
ii Kushindwa kulimudu darasa au kulitawala
kwa sababu pengine wameshamzoea mwalimu
wao huwa anawachapa hivyo ~~wao~~ wanafunzi
wanaamini ~~k~~ mgeni hawezi kuwachapa.
iii Wanafunzi kutokulielewa somo: Kutokana na njia
ambazo wamekwisha ~~zizoea~~ mfano maswali na
na majibu.
iv. Wanafunzi kuogopa kuuliza maswali. Kutoka
na na hawajamzoea anayewafundisha

**Kielelezo Na.10.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 10.

Aidha, watahiniwa 615 sawa na asilimia (17.0%) walipata alama za wastani katika swali hili kwani walikuwa na uelewa usiojitosheleza wa kukidhi matakwa ya swali. Hivyo, baadhi yao waliweza kuchambua changamoto 1 hadi 2 za kutumia mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji kwa usahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *mwanafunzi huweza kujenga hofu (woga), mgeni aliyealikwa anaweza kuchelewa kufika kwa ule muda waliokubaliana na mwalimu mwenyeji, huweza kutumia gharama* na *huweza kuwa mbinu hatarishi kwani mgeni anaweza kupata ajali njiani wakati wa kuja shuleni.* Hivyo, katika majibu hayo mtahiniwa alitoa majibu sahihi katika hoja ya kwanza na majibu dhaifu katika hoja ya pili, ya tatu na ya nne hivyo, kupata alama ya wastani.

Kwa upande mwingine takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 64 (1.8%) walifanya swali hili na kupata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mbinu anuai za kufundishia na kujifunzia Kiswahili. Hivyo, walishindwa kuchambua changamoto zinazoweza kujitokeza iwapo mwalimu atatumia mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, badala ya watahiniwa kuonesha chamngamoto za kutumia mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji kama vile: *kushindwa kuchukua nukuu za mada zilizotolewa kwa wanafunzi wenye umri mdogo, ushirikishwaji wa wanafunzi darasani unaweza kuwa mdogo hasa kama mgeni akiwa hana*

*mbinu za bora za mawasiliano, ufafanuzi unaotolewa na mgeni unaweza kutumia muda mrefu kama akiwa siyo mtunza muda* na *ikiwa mgeni siyo mwalimu anaweza kushindwa kulitawala darasa na kusababisha wanafunzi kushindwa kuelewa somo husika*. Mtahiniwa mmoja alitoa hoja dhaifu kama vile: *Wanafunzi kumcheka mwalimu anayewafundisha muda wote*, *ukosefu wa mwalimu kutopata maarifa ya kutosha kutoka kwa mwalimu mgeni, mwalimu kutokuwa mbunifu wa kutafuta njia na mbinu kufundishia na kujifunzia kutoka kwa mwalimu mgeni* na *wanafunzi kutokuwa wadadisi wa kutafuta maarifa kwa kina*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile: *uharibifu wa miundo mbinu, huweza kusababisha ugonvi kwa wanafunzi, wageni na wenyeji, husababisha upendeleo wa kujibu maswali* na *uchafuzi wa mazingira katika eneo la kujifunzia na kufundishia*. Watahiniwa wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kuandika faida ya kutumia mbinu hiyo badala ya changamoto zake. Kwa ujumla, majibu ya watahiniwa hao yanathibitisha kuwa watahiniwa wachache hawakuwa na umahiri wa kutosha juu ya mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la kiswahili. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa jibu sahihi katika swali husika.


10

i) Ukosefu wa kuongeza maarifa zaidi.
Mwalimu anapofundisha yeye muda wote vipo vitu hanavikosa na kuonekana ni wa kawaida mara zote awapo kwa wanafunzi.

ii) Ukosefu wa ushindani katika somo la Kiswahili.
Hii ni changamoto maana eli somo lipande mwango anafakuwa awepo mtu wa kumpa mwalimu changamoto zinazompanya awe imara

iii) Wanafunzi hujifunza kwa mazoea.
Wanaona hamna kipya na mwalimu ni yuleyule kwa eyo hufanya vyovyote.

iv) Ukosefu wa kuendana na hali iliyopo katika elimu.

**Kielelezo Na.10.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 10.


Kielelezo Na. 10.2 ni majibu ya mtahiniwa ambaye alielezea hasara za mwalimu kutotumia mbinu ya kualika mgeni badala ya changamoto zinazoweza kujitokeza iwapo mwalimu atafundisha kwa kutumia mbinu ya kualika mgeni.

### 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambayo yalitungwa kutoka katika mada ya *Utungaji, Stadi za Lugha,Upimaji* na *Maandalizi ya Kufundisha somo la Kiswahili.* Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote (4) ambapo kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama sitini (60). Vilevile, ufaulu wa watahiniwa umegawanyika katika makundi matatu. Mtahiniwa alibainishwa kuwa na kiwango hafifu cha ufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, wastani endapo alipata alama 6 hadi 10 na alihesabika kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu iwapo alipata alama 10.5 hadi 15.

#### 2.2.1 Swali la 11: Utungaji


Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kuandika barua ya kirafiki ambapo (100%) ya watahiniwa walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 80.3 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15. Chati Na. 11 inafafanua viwango hivyo vya ufaulu.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Watahiniwa 1,681 (46.5%) walijibu swali hili na kupata alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao, walikuwa na umahiri na maarifa ya kutosha katika kuandika barua ya kirafiki. Hivyo, waliweza kuonesha vipengele vyote muhimu vya barua husika kama vile, *anuani, tarehe, mwanzo wa barua/salam, barua yenyewe, mwisho wa barua* na *jina la mwandishi*. Aidha, watahiniwa hao waliweza kuandika kwa usahihi barua yenye vipengele hivyo kwa kuzingatia maudhui ya barua waliyopewa kwenye

swali husika. Kielelezo Na 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika kwa usahihi barua ya kirafiki.


11

BARUA YA KIRAFIKI

S.L.P 218,
Katavi.

12/05/2022.

Mpendwa Alfa Mkanjunju,
Ni matumaini yangu u mzima na buheri wa afya. Na kwa upande wangu witie shaka naendelea vizuri kabisa pamoja na majukumu ya kila siku.
Dhumuni langu ni kukupa taarifa kuwa nimeweza kupata uhamisho wa kikazi huku Katavi, ambapo isinge kuwa vizuri kuondoka bila kutoa taarifa yoyote.
Ningependa uwatadrifu nyumbani pia mklimie shangazi, mjomba pamoja na wote wanonifahamu. Na ningependa kuwakaribisha sana Katavi.

Wako mpendwa rafiki,
M. Mengi.
Mafuniko Mengi.


**Kielelezo Na.11.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 11.

Vilevile, watahiniwa 1,223 (33.8%) walijibu swali hili na kupata alama 6 hadi 10. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa yasiyojitosheleza juu ya uandishi wa barua ya kirafiki. Hivyo, waliandika barua bila kuzingatia muundo wa barua ya kirafiki katika baadhi ya vipengele vya barua husika na kusababisha kupata alama za wastani.

Hata hivyo uchambuzi unaonesha kuwa, watahini 713 (19.7%) walijibu swali hili na kupata alama 0 hadi 5.5. Wengi wao, hawakuwa na maarifa ya

kutosha juu ya uandishi wa barua ya kirafiki kwani hawakuwa na uelewa kuwa barua ya kirafiki huwa na vipengele kama vile: *anuani, tarehe, mwanzo wa barua/salam, barua yenyewe, mwisho wa barua* na *jina la mwandishi*.

Aidha, watahiniwa wengine waliandika barua ya kikazi badala ya barua ya kirafiki kama yalivyokuwa matakwa ya swali kama vile, *anuani ya mwandishi, tarehe, anuani ya mwandikiwa, kichwa cha barua, utangulizi, barua yenyewe, hitimisho, saini ya mwandishi* na *jina la mwandishi*. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali husika.


11.

MAFUNIKO MENGI,
S.L.P 218,
KATAVI,
12.05.2022.

ALFA MKANJUNJU,
S.L.P 18
MWANZA.
12.05.2022.

X YAH: TAARIFA YA KUHAMIA KATAVI KIKAZI.

Huika ni kichwa cha habari hapo juu.
Ni matumaini yangu kuwa u mzima wa afya na-
mimi pia sijambo naendelea vizuri na shughuli-
za kazi yangu. Dhumuni la kukuandikia barua-
hii ni kukupa taarifa kuwa nimehamia katavi-
kikazi hivyo bai nikipata likizo ya mwezi-
wa sita nitakuja kukucalimia rafiki yangu. Niku
takie majukumu mema, tuombe uzima tutaonana-
pale nitakapo pata mapumziko.
Ni mimi rafiki yako mpendwa.


MAFANIKIO MENGI.

**Kielelezo Na.11.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 11.

Kielelezo Na. 11.2, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali ambapo aliandika barua ya kikazi badala ya barua ya kirafiki hivyo kupata alama za kiwango hafifu.

### 2.2.2 Swali la 12: Stadi za Lugha

Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja tatu, kuonesha changamoto anazozipata mwalimu anayefundisha stadi za kuzungumza na kusikiliza na namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Watahiniwa wote asilimia 100 walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 92.2 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,119 (30.9%) walijibu swali hili na kupata alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Stadi za kuzungumza na kusikiliza. Hivyo, waliweza kuonesha changamoto tatu, anazozipata mwalimu anayefundisha stadi za kuzungumza na kusikiliza na namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja za changamoto kama vile: *wanafunzi wanaulemavu katika ala za sauti, athali ya lugha mama kwa mwalimu na mwanafunzi* na *wanafunzi kushindwa kupangilia maneno hivyo kushindwa kuunda sentensi sahihi.* Aidha, kwa upande wa namna ya kutatua changamoto hizo alieleza hoja kama vile: *mwalimu mwenyewe afanye mazoezi kutokana na kasoro alizonazo, inashauriwa wanafunzi wenye ulemavu kama bubu na viziwi wapelekwe kwenye shule maalumu* na *mwalimu atoe mazoezi mbalimbali ya*

*kutamka maneno*. Vilevile, mwanafunzi mwingine alitoa hoja kama vile: *kasoro katika maumbile mfano usikivu hafifu, athali za lugha mama* na *wanafunzi kushindwa kuunganisha maneno hivyo, kushindwa kutamka maneno kwa usahihi*. Aidha, mtahiniwa huyo alionesha namna ya kutatua changamoto hizo kuwa ni: *wanafunzi wenye kasoro katika maumbile kama vile usikivu hafifu mwalimu anatakiwa kuweka msisitizo au mkazo kwa wanafunzi hao katika kuandika kwa usahihi na kutumia vifaa vya tiba matamshi.* Wenye changamoto ya *athali ya lugha mama, mwalimu anatakiwa kuwapa wanafunzi mazoezi mengi ya utamkaji wa sauti, maneno na sentensi*. Pia kwa wanafunzi wenye changamoto ya *kushindwa kutamka maneno kwa usahihi. Mwalimu anatakiwa kurekebisha kasoro hiyo mara kwa mara baada ya mwanafunzi anapokosea utamkaji wa hayo maneno*. Kwa ujumla watahiniwa hao waliweza kujibu kwa usahihi na kutoa utangulizi na hitimisho zuri linaloendana na matakwa ya swali hivyo, kupata alama za kiwango kizuri. Kielelezo Na. 12.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi.

12 Stadi ya Kuzungumza ni uwezo wa
kutamka maneno kwa kutoa sauti ili kufikisha
ujumbe, lakini stadi ya kusikiliza ni uwezo
wa kupokea mawimbi ya sauti kupitia mlango
wa fahamu sikio na kuweza kupata ujumbe
uliokusudiwa, zifuatazo ni changamoto
zitakazomkabili mwalimu anayefundisha
stadi ya kuzungumza na kusikiliza:-

Kasoro katika maumbile mfano
usikivu hafifu, kukosa baadhi ya ala za sauti
kutokana na kithembe na kigugumizi. Mwalimu
anayefundisha stadi ya kuzungumza na kusikiliza
huweza kukabiliana na wanafunzi wenye
kasoro katika maumbile mfano usikivu hafifu
ambao humzuia mwanafunzi kupata ujumbe
uliokusudiwa pamoja na ukosefu wa baadhi ya
ala za sauti ambao humfanya wanafunzi
washindwe kutamka maneno kwa ufasaha.


Athari za lugha mama; wanafunzi
wengi wameathiriwa na lugha zao za mwanzo
(lugha mama) ambazo huweza kuwapa changam-
oto katika kutamka baadhi ya maneno
Mfano wakurya ~~kutamka~~ kusema kurara baadale
ya kulala, wachaga kusema fiatu baadale ya
~~vit~~ viatu na wasukuma kusema marazi baadale
ya maradhi. Hivyo mwalimu huweza kupata
changamoto ya wanafunzi kushindwa kutamka
maneno kwa ufasaha wakati wa kufundisha
stadi ya kuzungumza na kusikiliza.

Wanafunzi kushindwa kuunganisha
maneno hivyo kushindwa kutamka sentensi kwa
ufasaha; vilevile ~~mwanafunzi~~ mwalimu hukabiliana

**Kielelezo Na.12.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 12.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 2,216 (61.3%) walijibu swali hili na kupata alama za wastani ambazo ni kuanzia 6 hadi 10 kwani walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Stadi za Lugha*. Hivyo, walishindwa kufafanua hoja zao kwa kina juu ya changamoto anazozipata mwalimu anayefundisha Stadi za kuzungumza na kusikiliza na namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Baadhi yao waliishia kutaja changamoto tu na kushindwa kufafanua changamoto hizo na namna ya kuzitatua. Watahiniwa wengine, walifafanua hoja 2 hadi 3 na kushindwa kufafanua namna ya kutatua changamoto hizo. Vilevile, watahiniwa wengine walishindwa kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho sahihi badala yake walirudia swali katika sehemu ya utangulizi na wengine kuorodhesha hoja walizojadili kwenye kiini cha insha hivyo, kusababisha kupata alama za wastani.

Pamoja na hayo, watahiniwa 286 (7.8%) walipata alama hafifu 0 hadi 5.5 kutokana na kukosa umahiri na maarifa kuhusiana na mada ndogo ya *Stadi za kuzungumza na kusikiliza*. Hivyo, kushindwa kufafanua changamoto anayoipata mwalimu anayefundisha Stadi za kuzungumza na kusikiliza na namna ya kukabiliana nazo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika changamoto za jumla anazokutana nazo mwalimu anapofundisha somo lolote badala ya kufafanua changamoto anazoweza kukutana nazo mwalimu anayefundisha stadi ya kuzungumza na kusikiliza. Mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile: *mwanafunzi kukosa utashi na utayari wa kusoma, mwalimu kukosa vifaa vya ujifunzaji na kufundishia* na *kutokuwa na mazingira chanya ya kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji*. Aidha, katika kukabiliana na changamoto hizo mtahiniwa huyo alitoa hoja ambazo ni: *kutumia mbinu shirikishi katika kufundishia, kutumia muda wa ziada katika kufundisha* na *kutumia andalio la somo katika kufundishia*. Mtahiniwa mwingine alitoa changamoto kama vile: *Wanafunzi kutotumia ishara, wanafunzi kutozingatia maelekezo ya mwalimu* na *kutokuwa na shauku ya kuuliza maswali darasani.* Kwa upande wa kutatua changamoto alitoa hoja kama vile, *kutumia ishara, wanafunzi kuzingatia maelekezo ya mwalimu* na *kuwa na shauku ya kuuliza maswali darasani*. Hata hivyo, watahiniwa hao walishindwa kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na swali hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo Na 12.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


12

Mwalimu anayefundisha stadi ~~za~~ kuzungumza na kusikiliza.

Stadi za kuzungumza: Ni aina ya stadi ya Lugha inayotumia mazungumzo:

Stadi za Kusikiliza: Ni aina ya stadi ya Lugha inayotumia kusikiliza:

Zifuatazo ni changamoto zinazomkabili mwalimu anayefundisha stadi ya kuzungumza na kusikiliza:

Wanafunzi kutokutumia Lugha sanifu: Hii ni changamoto mojawapo humkabili mwalimu wakati anafundisha stadi ya kuzungumza na kusikiliza kwahiyo changamoto ya utamkaji wa herufi.

Wanafunzi kutokuzingatia alama za Uandishi au za Lugha: Hii ni changamoto mojawapo humkabili mwalimu wakati wa kufundisha ~~stady~~ stadi ya kuzungumza na kusikiliza.

Kutokuwa na utulivu darasani: Hii ni changamoto nyingine inamkabili mwanafunzi wakati anafundisha stadi ~~za~~ za kuzungumza na ~~kujif~~ kusikiliza kutokuwa na utulivu darasani hii ni changamoto kwa mwalimu wakati anafundisha:

Zifuatazo ni namna ya kukabiliana na changamoto wakati wa kufundisha stadi za kuzungumza na kusikiliza darasani:

wanafunzi ~~x~~ Kutumia Lugha sanifu au fasaha: Hii ni namna ya kukabiliana na changamoto hizo kutumia Lugha fasaha wakati wa kuzungumza hii inaweza ikamsaidia mwalimu kurahisisha mchakato wa ufundishaji na


**Kielelezo Na.12.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 12.

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali kwa kuonesha namna za jumla za kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo lolote badala ya

kuzingatia stadi ya kuzungumza na kusikiliza kama yalivyokuwa matakwa ya swali.


### 2.2.3 Swali la 13: Upimaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza faida tano za upimaji kwa mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Watahiniwa wote (100%) walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 99.4 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika chati Na. 13.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu kwa Watahiniwa katika Swali la 13*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 3,295 (91.1%) walifanya mtihani na kupata alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na dhana ya upimaji hivyo, walielezea faida 4 hadi 5 za upimaji kwa mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Mfano mtahiniwa mmoja, alitoa hoja kama vile: *husaidia kujua maendeleo ya mwanafunzi katika somo la Kiswahili, humsaidia kujua matatizo ya mwanafunzi katika ujifunzaji*, *husaidia kumpangia mwanafunzi nafasi* na vilevile *humsaidia kuchochea ari ya mwanafunzi kujisomea*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile, *kufahamu kiwango cha maendeleo ya mwanafunzi, kufahamu changamoto anazokumbana nazo mwanafunzi, kuweza kufahamu sehemu zinazoitaji marekebisho na maboresho, saidia mwalimu kuboresha mbinu na zana* na *ufundishaji na husaidia kupata vyeti mbalimbali.* Kwa ujumla watahiniwa hao walikuwa na umahiri mkubwa wa kujua faida katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na 13.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa alijejibu kwa usahihi.


13 Upimaji: Ni mchakato wa kupima stadi, mwenendo na maarifa ya wanafunzi katika ujifunzaji wake. Kuna aina za Upimaji nazo ni Upimaji awali, upimaji endelevu, Upimaji gunduzi na Upimaji tamati. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji una faida mbalimbali nazo ni:

Kubaini maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji wake: Mwalimu wa somo anapofanya Upimaji anabaini maendeleo ya wanafunzi pia maendeleo ya mwanafunzi mmoja mmoja katika ujifunzaji wake. Mfano Mwanafunzi alikuwa hajibu maswali, mwanafunzi alikuwa hawezi kuumba herufi vizuri, Lakini kutokana na Upimaji ameweza kugundua mwanafunzi ameweza kupiga hatua katika ujifunzaji wake.

Unamsaidia Mwalimu kufanya tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji: kutokana na kufanya Upimaji anaweza kufanya tathmini kwa namna gani amefanikiwa katika mchakato wa Ufundishaji au ameweza kutambua kiwango cha kinachojitokeza na mwanafunzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.


Umsaidia Mwanafunzi kupanda Ngazi moja kwenda kazi Nyingine ya kielimu: Mfano mtihani wa Necta mwanafunzi anapanda kazi moja kwenda nyingine baada ya kufanyiwa Upimaji wa mtihani wa necta hivyo basi unaweza kumuhamasisha mwanaf

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 13.

Kielelezo Na 13.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa 299 (8.3%) walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10 kwani walikuwa na uelewa wa wastani katika mada ya *Upimaji*. Hivyo, walitoa faida zisizojitosheleza za upimaji kwa mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kwa mfano, baadhi yao waliishia kutaja faida tu na kushindwa kufafanua faida hizo na wengine walifafanua faida 2 hadi 3 na kushindwa kutoa maelezo kwa usahihi yanayoendana na matakwa ya swali. Vilevile, wapo watahiniwa walioshindwa kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho kwa usahihi hivyo, kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa 23 (0.6%) walijibu swali hili na kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5 kwani walikosa umahiri na maarifa kuhusu mada ya *Upimaji*. Hivyo, kushindwa kueleza faida tano za upimaji kwa mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Baadhi yao walitoa faida 2 hadi 3 bila kuzifafanua na kushindwa kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na swali. Aidha, watahiniwa wengine walifafanua hoja ambazo ni dhaifu kama vile: *humsaidia mwalimu kufanya mazoezi, humjengea mwanafunzi kuwa muoga, humjenge mwalimu na mwanafunzi uadui, humjengea mwanafunzi dadisi na humjengea mwanafunzi utoro siku za mitihani*. Pia, watahiniwa wengine walishindwa kueleza faida za upimaji kwa mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji badala yake wakaelekeza majibu yao kwa walimu pekee na kusababisha kupata alama dhaifu. Kielelezo Na 13.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.



13

Upimaji ni uwezo au utaratibu ambao mwalimu huweza kuufanya kwa wanafunzi wake ili kuweza. Kutambua ni kwa kiwango gani umeweza kueleweka vizuri kile alicho weza kufundishwa na wangapi awajaweza kueleweka. Kuna aina mbalimbali za upimaji mfano upimaji awali, upimaji endelevu, upimaji gunduzi na upimaji tamati. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili una faida mbalimbali ambazo ni

Humsaidia mwalimu kufanya tathimini, mfano mwalimu anawapa wanafunzi mitihani mbalimbali ya mihula lengo kuu ni kutambua uwezo wa wanafunzi kutaka kuelewa ni kwa kiwango gani wameeleweka au kufanya vizuri na wale ambao wameweza kufanya vibaya, mwalimu hutumia mbinu na njia mbalimbali za kuwaelimisha vizuri hivyo upimaji ni muhimu sana.

Humjengea mwanafunzi kujiamini zaidi, mfano - kujibu maswali mbalimbali, kujieleza, kusoma, na mengineyo Upimaji ni muhimu sana kwa mwalimu na mwanafunzi huiwani katika swala zima la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kujiamini ni muhimu sana na vizuri kwani humjengea stadi mbalimbali kukabiliana nazo kutaka na na kujiamini kwake hivyo inashauriwa kujiamini ni vizuri huiwani katika maisha.

Humjengea mwalimu na mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu. Upimaji ni muhimu sana huiwani katika swala zima la ufundishaji na ujifunzaji hii huweza kuwafanya wanafunzi kuwa na kumbukumbu nzuri kulingana na upimaji ambao mwalimu huweza kuutumia kwani ni muhimu sana mwalimu kuwa na kumbukumbu ya kudumu kulingana na upimaji ambao huufanya.


Humjengea mwanafunzi stadi mbalimbali. Upimaji ni muhimu sana kwa mwalimu na mwanafunzi kwa ujumla

**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 13.

Kielelezo Na 13.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea baadhi ya hoja zinazoonesha umuhimu wa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia badala ya faida za upimaji kwa mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

### 2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja tano kuthibitisha kauli isemayo "Utaaluma na taaluma ya mwalimu haitoshi kumfanya afundishe bila andalio la somo". Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango kizuri kwani asilimia 99.6 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15 kama inavyofafanuliwa katika chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 3,414 (94.4%) walijibu swali hili vizuri na kupata alama 10.5 hadi 15 kwani walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa andalio la somo katika ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa katika kundi hili, waliweza kueleza faida 4 hadi 5 za matumizi ya andalio la somo kama ifuatavyo: *humwezesha mwalimu kutumia kwa ufanisi muda uliopangwa kufundishia, humpa mwalimu mwingine anayefanya kazi hiyo badala wa yule wa awali msingi wa kuwasilisha somo, humuongoza mwalimu kufanya tathmini ya ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji, kuonesha wazi malengo ambayo mwalim anatarajia yafikiwe na mwanafunzi* na *humuonesha mwalimu umahiri unaopashwa kufikiwa kwa kujifunza mada husika.* Kielelezo Na 14.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali kwa usahihi.

14 Andalio la somo, Ni mpango wa muda mfupi ambao hutumiwa katika kipindi husika. Huandaliwa kila siku.

Ufuatao ni Umuhimu wa andalio la somo kwa mwalimu.

Humsaidia mwalimu kufundisha kwa mtiririko; Andalio la somo ni muhimu kwani sababu mojawapo ni kumfanya mwalimu afundishe kwa mtiririko mzuri anapokuwa darasani.

Humsaidia mwalimu kubaini zana atakazotumia; Pia andalio la somo humwezesha mwalimu kubaini zana za kufundishia na kujifunzia atakazotumia mwalimu ili aweze kufundisha kwa ufanisi.

Humsaidia mwalimu kufundisha kwa kujiamini; Vile vile andalio la somo ni muhimu, kwani humfanya mwalimu aweze kufundisha kwa kujiamini anapokuwa darasani akiwasilisha maarifa yake.


Humsaidia mwalimu kubaini zana za Upimaji; Pia katika kipengele cha ~~kukazia~~ hitimisho maarifa katika hatua za somo huweza kumpa mwongozo mwalimu kuwa atatumia zana zipi za Upimaji. Mfano, Maswali na majibu, Zoezi au jaribio

Humsaidia mwalimu kubaini mbinu zitakazotumika katika ufundishaji na Ujifunzaji; Pia andalio la somo humsaidia mwalimu kubaini mbinu na njia atakazotumia katika ufundishaji na Ujifunzaji wa somo husika. Mfano Majadiliano, Onesho mbinu

**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 14.

Hata hivyo, watahiniwa 187 (5.2%) walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao, walikuwa na uelewa wa wastani juu ya umuhimu wa kutumia andalio la somo katika kufundishia na kujifunzia. Baadhi yao walitoa hoja 2 hadi 3 badala ya 5 kama yalivyokuwa maelekezo ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua hoja kama vile: *andalio la kazi hutoa nukuu za somo husika, husaidia mwalimu kupata zana za kufundishia* na *husaidia kurejerea maandiko.* Aidha, watahiniwa wengine waliweza kuonesha faida za kutumia andalio la somo na kushindwa kufafanua kwa kina faida hizo. Hii ilisababisha watahiniwa hao kupata alama za wastani.

Licha ya watahiniwa wengi kufanya vizuri swali hili, wapo watahiniwa 16 (0.4%) walijibu vibaya na kupata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hao, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* hususani katika kipengele cha andalio la somo. Baadhi yao, walijibu kinyume na matakwa ya swali na wengine kutoa hoja ambazo sio sahihi. Mfano, mtahiniwa mmoja badala ya kuelezea faida ya kutumia andalio la somo alielezea hasara ya mwalimu kufundisha bila kutumia andalio la somo kama vile, *kutoka nje mada husika, kutofikia malengo ya ufundishaji, kuruka baadhi ya vitu muhimu katika ufundishaji* na *kutumia muda mrefu katika kufafanua kitu kimoja*. Vilevile, mtahiniwa mwingine alieleza vipengele muhimu vinavyounda andalio la somo kama vile: *utangulizi, zana za ufundishaji, vitabu vya marejeo, kukazia maarifa* na *kutoa mazoezi*. Kielelezo Na 14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea kwa usahihi faida za mwalimu kutumia andalio la somo.


14 Andalio la somo: Ni mpango kazi wa m
uda mfupi unaoandaliwa na Mwalimu ili kumwongo
za katika suala zima la ufundishaji na ujifunza
ji ndani ya muda wa kipindi cha siku moja, wiki au mwezi.
pia andalio la somo lina vipengele muhimu vya
kufuata kama utangulizi, kujenga umahiri, kuimari
sha umahiri na hitimisho.
Yafuatayo ni mambo yanayompanya Mwali
mu afundishe bila andalio la somo:
Utayari wa Mwalimu: Tunaona Mwalimu
asipokuwa na utayari katika kufundisha itamf
anya kutoandaa andalio la somo kwa sababu
hana utayari wa kufanya hilo jambo.
Mwingiliano wa majukumu kazini: Una
kuta Mwalimu amepewa majukumu mengi shuleni
na anatakiwa ayakamilishe na aingie darasani
hivyo Mwalimu atafanya majukumu aliyopewa na
baadae atashindwa kuandaa andalio la somo na
kumpelekea kwenda kufundisha bila ya kutumia
andalio la somo.
uvivu: Tunaona Walimu wengi ni wavivu
kazini katika kuandaa vipaa vya mtaala ikiwemo an
dalio na wengine huchelewa shuleni kwa ajili ya u
vivu wa kuamka mapema hivyo anapofika shuleni
amechelewa na muda wa kufundisha umefika hu
shindwa kuandaa andalio la somo na kwenda kuf
undisha bila kutumia andalio la somo.
Kukata tamaa: pia Walimu wengi wanak
ata tamaa hasa wanapokuwa wanafundisha na
wanakata tamaa kutokana na sababu kama vile
kulipwa ujira mdogo, kupewa kazi nyingi na weng
ozi wa shule kwa wakati mmoja hivyo inapelekea

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 14.

Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutafsiri matakwa ya swali hivyo, badala ya kuelezea faida ya kutumia andalio la somo alieleza mambo yanayosababisha mwalimu kufundisha bila andalio la somo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa Cheti cha Ualimu Daraja la A wa Somo la Kiswahili ulikuwa na maswali 14 yaliyotungwa kutoka katika mada 9. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa walifanya vizuri katika mada 6 ambazo ni sawa na asilimia 60.4 ya mada zote zilizotahiniwa. Mada hizo ni; *Upimaji (99.4%), Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia (97.6%), Zana za kufundishia na kujifunzia* (95.4%), *Sarufi (88.2%), Uchambuzi wa vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili (82.5%)* na *Stadi za Lugha (79.9%).* Mada hizo zilikuwa na ufaulu wa kiwango kizuri kwa sababu watahiniwa wengi walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika na kuelewa matakwa ya kila swali. Aidha, waliweza kujieleza kwa ufasaha na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hasa katika maswali ya insha.

Vilevile, watahiniwa walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu katika mada tatu ambazo ni sawa na asilimia 17.9 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni: *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili (58.1.%), Utungaji (55.0) na Fasihi Simulizi* (48.1%).

Uchambuzi zaidi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada zilizotahiniwa unaonesha kuwa hakukuwa na mada iliyokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu ikilinganishwa na ufaulu wa mada mwaka 2021. Kwa mwaka 2021 kulikuwa na mada mbili ambazo zilikuwa na viwango hafifu vya ufaulu. Mada hizo ni *Zana za Kufundishia na Kujifunzia (36.8%) na Matamshi na Lafudhi (26.7%).*

Aidha, kiwango cha ufaulu katika mada ya *Upimaji*, *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia* pamoja na *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* vimepanda. Kwa mwaka 2021 mada hizo zilikuwa na ufaulu wa asilimia 63.3, 70.7 na 36.8 na mwaka 2022 zimekuwa na asilimia 99.4, 97.8 na 95.4 mtawalia. Hivyo, kumekuwa na ongezeko la asilimia 36.1, 27.3 na 58.6 ikilinganishwa na ufaulu wa mada hizo kwa mwaka 2021.

## 4.0 HITIMISHO

Taarifa hii inaonesha kuwa, watahiniwa wamefaulu kwa kiwango kizuri katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2022 kwani asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu. Aidha, watahiniwa wamefaulu kwa kiwango hicho kwa kuwa walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa na kuelewa matakwa ya maswali mbalimbali.

Licha ya watahiniwa kufaulu kwa kiwango cha juu, juhudi zinahitajika katika kuimarisha uelewa wa mada zilizokuwa na ufaulu wa wasatani ambazo ni: U*tungaji*, *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili* na *Fasihi Simulizi* ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kwa mitihani ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ufaulu wa watahiniwa katika somo la Kiswahili ulikuwa mzuri kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali, wadau mbalimbali wa elimu pamoja na wakufunzi katika kuhakikisha kuwa kiwango cha umahiri kinaongezeka. Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika somo hili inashauriwa:

(a) wakufunzi watumie njia ya igizo dhima, onesho mbinu pamoja na vikundi katika ufundishaji wa mada ya *Fasihi Simulizi* ili kuwasaidia walimu tarajali kufahamu semi, sanaa za maonesho na wahusika mbalimbali katika hadithi.

(b) wakufunzi watumie mbinu za mihadhara mifupi, majadiliano ya jumla ya maswali na majibu na mazoezi ya kuandika, kuzungumza, majaribio na mkoba wa kazi katika kufundisha mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* ili walimu tarajali wajifunze kwa vitendo.

(c) wakufunzi wawaongoze walimu tarajali kufanya mazoezi ya kina katika mada ya utungaji hasa katika kipengele cha uandishi wa barua za kirafiki kwa kutumia barua halisi na kadi za manila zinazoonesha vipengele vya barua ya kirafiki ili kuwajengea uwezo zaidi walimu tarajali kuelewa muundo wa barua ya kirafiki.

(d) walimu tarajali wapewe mazoezi ya kujibu maswali mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wa kubaini matakwa ya swali. Aidha, wapewe

mrejesho kuhusu namna walivyojibu maswali husika ili kuwajengea uwezo zaidi.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

| Na. | Mada | Namba ya swali | Viwango vya Kufaulu (%) | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 40 na Zaidi | Wastani | |
| 1. | Upimaji | 13 | 99.4 | 99.4 | Vizuri |
| 2. | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia | 6 | 97.7 | 98.0 | Vizuri |
| | | 10 | 98.2 | | |
| 3. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 8 | 95.4 | 95.4 | Vizuri |
| 4. | Sarufi | 3 | 99.9 | 88.2 | Vizuri |
| | | 5 | 76.5 | | |
| 5. | Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili | 7 | 82.5 | 82.5 | Vizuri |
| 6. | Stadi ya Lugha | 1 | 67.5 | 79.9 | Vizuri |
| | | 12 | 92.2 | | |
| 7. | Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili | 9 | 16.6 | 58.1 | Wastani |
| | | 14 | 99.6 | | |
| 8. | Utungaji | 4 | 29.6 | 55.0 | Wastani |
| | | 11 | 80.3 | | |
| 9. | Fasihi Simulizi | 2 | 48.1 | 48.1 | Wastani |